

Jicho la pili kuhusu sakata la mkonge

NA MWANDISHI WETU

MACHI Mosi mwaka huu, Tume ya Uchunguzi iliyoteuliwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (MB), ilitoa taarifa yake kwenye kikao cha Viongozi na Watendaji, wa Mkoa wa Tanga, kilichoitishwa na Waziri Mkuu.

Katika taarifa hiyo, shutuma mbalimbali zilitolewa dhidi ya Katani Limited, baadhi ya viongozi wake wakuu, wakurugenzi wa bodi na wanahisa.

Miongoni mwa shutuma hizo ni pamoja na ubinafsishaji wa iliyokuwa Mamlaka ya Mkonge Tanzania kutofuata utaratibu, uharibifu wa rasilimali, mitambo na miundombinu pamoja na kupora mali za MMT kama nyumba za kuishi, n.k.

Tuhuma hizi ni kubwa na nzito, lakini jamii haikupata nafasi kusikiliza upande wa pili wa shilingi, yaani watuhumiwa, hivyo kama mda wa katani na ninayejua historia hiyo vizuri, nimeamua kueleza jicho la pili la sakata hilo.

Kwa maoni yangu ili haki sio tu itendeke, bali ionekane kuwa imetendeka, taarifa ile ya Tume ipewe watuhumiwa ili waweze kutoa maelezo na vielelezo vya kuthibitisha kuwa ubinafsishaji wa Mamlaka ya Mkonge Tanzania, ulitekelezwa kwa kufuata taratibu zote za wakati huo chini ya ile iliyokuwa inajulikana kama Presidential Parastatal Sector Reform Commission (PSRC).

Aidha, mchakato wa ubinafsishaji wa Mamlaka ya Mkonge Tanzania, ulipitiwa na wizara kadhaa kati ya mwaka 1996 hadi mwaka 2005; Baraza la Mawaziri mara tatu na Baraza la Usuluhishi (Arbitral Tribunal), ambayo wajumbe wake waliokuwa ni Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Jaji Joseph Warioba, Wakili Mohamed Ismail na Wakili Peter Bakilana (Arbitrators).

Kuna mikataba na makubaliano kati ya Serikali na Katani Ltd, kampuni inayomilikiwa na Watanzania 87 wazawa waliokuwa wafanyakazi wa Mamlaka ya Mkonge Tanzania.

Haiwezekani kwamba mikutano mitatu ya Baraza la Mawaziri, wizara kadhaa pamoja na Baraza la Usuluhishi wote washindwe kuziona dosari hizo zilizoko kwenye Taarifa ya Waziri Mkuu.

Watuhumiwa wanadai kwamba wangeipata taarifa hiyo wangeleza kutoa maelezo ambayo yangeondoa wasiwasi wowote kuhusu suala zima la ubinafsishaji.

MAFANIKIO YA KATANI

Kuna ushahidi usikuwa na chembe ya shaka, kwamba Katani Ltd imepata mafanikio mazuri.

Uzalishaji umepanda kutoka tani 849 mwaka 2005 hadi tani 5,420 mwaka 2017. Iliasisi mfumo wa uzalishaji mkonge

kwa wakulima wadogo 2,100 kwenye mashamba matano mkoani Tanga.

Miongoni mwa wakulima hao wadogo ni baadhi ya wahariri wa vyombo vya habari ambao wanamiliki mashamba ya mkonge kwa utaratibu halali kabisa.

Katani imefufua viwanda saba vya kusindika mkonge na kukarabati na kupanua kiwanda cha kuzalisha bidhaa za mkonge cha Tancord na kukifanya kuwa kikubwa kupita vyote Afrika nzima; Ajira 5,200 zimetengen- ezwa.

Kampuni ya Katani ni walipaji wakubwa wa kodi mkoani Tanga, imeendeleza utafiti wa bidhaa za mkonge na ukulima wa mkonge ikiwa ni pamoja na kujenga kiwanda cha kwanza ulimwengu cha kuzalisha umeme na mbolea kutoka kwenye makapi ya majani ya mkonge baada ya usindikaji.

Katani Ltd imetayarisha mpango wa maendeleo ulioonesha kuwa Tanzania tunaweza kuzalisha tani 1,000,000 za mkonge na kuuza bidhaa zake katika soko la ndani na masoko mengine duniani. Haiingii akilini kuwa kampuni kama hii inaweza kuhujumu mkonge na rasilimali zake.

Kuna tuhuma kwamba Katani Limited ilikopesha pesa kampuni ya Tanzania Pharmaceutical Industries Ltd pesa takriban shilingi milioni 470, kutokana na mkopo ambao Katani Ltd waliupata kutoka NSSF.

Ukweli ni kwamba kampuni hizi mbili, Katani Ltd na Tanzania Pharmaceutical Industries Ltd (TPI) ni Kampuni binafsi (Private Companies), ambazo zina mamlaka kamili ya kukopa na kukopesha, kushtaki na kushtakiwa. Ndio maana



Salum Shamte

Katani Ltd iliweza kukopa popote ilipokubalika.

Kampuni nyingi za binafsi (Private Companies) zina utaratibu wa kukopesha, iwe fedha na/au malighafi.

Kwa mantiki hiyo, Katani Ltd ilipokuwa na ukata na kukosa fedha za kuendesha mkutano wa Kimataifa wa Nyuzi Ngumu Asilia (International Conference on Hard Natural Fibres), ambapo Ndugu Salum Shamte alikuwa ni Mwenyekiti wa "FAO Conference on Hard Fibres"; na mkutano huo ulikuwa unafanyika Tanga, Tanzania, Katani iliomba mkopo kutoka TPI.

TPI ilikopesha Katani Ltd fedha hizo. Mkutano ukafanyika, na Katani ilipokuwa na ukwasi, walizirejesha fedha hizo.

Kadhalika TPI ilipopata dharura na kuhitaji kile kinachoitwa "bridging finance", iliomba mkopo kutoka Katani Ltd.

Katani Ltd ilitoa mkopo huo kwa TPI kwa riba ya asilimia 16.

TPI iliurejesha mkopo huo wote, ikiwa ni pamoja na riba. Uhusiano huu ulikuwa ni wa kibiasara na pande zote mbili zilinufaika. Na hiyo ndio biasara.

MATATIZO YALIANZIA HAPA

Matatizo makubwa ya Katani Ltd yalianza mwaka 2018 wakati Mkuu wa Mkoa wa Tanga alipolazimisha mfumo wa mauzo ya mkonge kupitia mnada na vyama vya ushirika - mfumo ambao hau- tumiki mahali popote duniani.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martin Shigella, alifungia kampuni ya Katani Ltd. isizalishe mkonge kwenye viwanda vyake vyote saba kwa miezi 5 mwaka 2018 na kuleta athari kubwa sana kwenye mapato ya wakulima, wafanyakazi, kampuni na kodi ya Serikali na mauzo ya nje ya zaidi ya shilingi bilioni 10.

Mfumo huu uliolazimishwa kwa nguvu bila ya matayarisho yoyote unawalazimisha wakulima ambao wanahisa kwenye viwanda kuuzia kampuni ya Kichina mkonge wao wote ambao wanaupeleka China na kukikopesha kiwanda cha Tancord malighafi ya kutengeneza bidhaa za mkonge. Hii ni kinyume kabisa na sera ya Taifa ya maendeleo ya viwanda.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga katika kuendeleza hatua za kuimiza kampuni ya Katani Ltd. aliamuru viongozi watano wakamatwe na Polisi na kuwaweka kizuizini Oktoba 2019 na wapo kizuizini mpaka leo.

Viongozi hao ni Salum Shamte (69), Mkurugenzi wa Bodi ya Katani Ltd; Fatma Riyami (66), Mkurugenzi wa bodi na Juma Shamte (44) ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji kwa tuhuma za kuchelewesha malipo ya wakulima.

Wengine wawili - Mkurugenzi wa Fedha -Fadhili Mhina na Katibu wa Bodi na Meneja Uhusiano Bibi

Theodora Mtejeta wako nje kwa dhamana.

Haleleweki kwa nini kina Shamte na Riyami wamenyimwa dhamana na kama kuna kesi yoyote ya jinai dhidi yao.

Zimetolewa tuhuma pia, zikielekezwa kwa Salum Shamte kwamba aliua nyumba (na pesa kutia mfukoni mwake), mali ya Mamlaka ya Mkonge Tanzania, iliyoko London na ambayo alikuwa akiishi alipokuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Tanganyika Sisal Marketing Association (TASMA).

Nyumba hiyo ya London ipo Edgware na Salum Shamte alipoondoka aliiacha mikononi mwa Ubalozi wa Tanzania. Ushahidi upo. Na mpaka leo kuna ofisa wa Ubalozi wa Tanzania nchini Uingereza anayekaa humo.

Nyumba ya Shamte anayokaa Tanga aliuziwa wakati wa ubinafsishaji, miaka ya 1990/2000.

Mauzo haya yalifanyika kihalali kama yaliyofanyika kwenye nyumba nyingine za Mashirika ya Umma yaliyobinafsishwa kama vile Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), Tanzania Breweries Limited, Tanzania Cigarette Company Limited, SIMU 2000 - kwa kuyataja baadhi tu ya mashirika.

Isitoshe, kuna nyumba nyingi ziliuzwa kwa wafanyakazi wa serikali na mashirika ya umma waliokuwa wanaishi kwenye nyumba hizo.

Hatuamini kuwa Serikali ina nia ya kuwanyang'anya maelfu ya Watanzania hao nyumba zao walizouziwa kihalali kutokana na maamuzi sahihi ya Serikali ya wakati huo. Wakijaribu kutunyang'anya nyumba zetu ni lazima tutakwenda mahakamani kupinga kwa nguvu zetu zote.



Shamba la mkonge.